Jarida la Mtandaoni

Tolea la 01

Julai - Septemba 2026



MWANZA

Yetu, Heshima Yetu

mwanza.go.tz || rs_mwanza

UHARIRI



Dkt. Fatuma Mganga
Katibu Tawala wa Mkoa
wa Mwanza

Mhariri

Paulo Zahoro
Afisa Habari wa Mkoa

Waandishi

Paulo Zahoro
Anthony Ramadhani

Wapiga Picha

Anthony Ramadhani
Innocent Hamidu
Bibiana Luchapa
Zainabu Omary
Debora Asangalwisye
Irene Kihwili

Msanifu wa Jarida

Yohannes Kayombo

Yaliyomo

iv Ujumbe kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. CP. Salum Hamduni

01 Serikali yazindua kituo cha operesheni na mawasiliano ya dharura Mwanza

02 Mwanza yaongeza kasi kuzuia vifo vya kuzama maji Ziwa Victoria

03 Sikukuu ya Wakulima (Nanenane) Mkoa wa Mwanza

04 Mwenge wa Uhuru waifikia miradi 51 ya shilingi bilioni 101.9 Mwanza

05 CP Hamduni akabidhiwa Rasmi Ofisi

06 RC Hamduni ashiriki usafi wa soko kuu la Mwanza, atoa onyo kwa watendaji na wafanyabiashara

07 Katibu Mkuu Maendeleo ya Jamii atembelea Ofisi za Mkuu wa Mkoa

08 Kamati za maafa Mwanza zatakiwa kuimarisha maandalizi ya kukabiliana na mvua za El Nino



UJUMBE KUTOKA KWA MKUU WA MKOA WA MWANZA, MHE. CP SALUM HAMDUNI

Ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza na ninawaahidi kutekeleza majukumu yangu kwa weledi mkubwa. Ninawasihi watumishi wote kuwatumikia wananchi kwa moyo wote, kuongeza ufanisi, na kusimamia ukusanyaji pamoja na matumizi ya mapato ya ndani kwa kufuata sheria na kanuni za fedha.

Nikiangazia sekta ya biashara, ninawasihi wafanyabiashara wadogo kufuata sheria na taratibu zilizopo. Wakati huo huo, nina-zielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha zinawapanga vema wafanyabiashara hao kwenye maeneo rasmi ili kuweka utaratibu mzuri na salama wa shughuli za kiuchumi.

Mwisho, ninaziagiza mamlaka husika na kamati za maafa kuimarisha usafi na kujiandaa vyema kukabili mvua za El Niño zinazotarajiwa mwezi Oktoba. Hatua hizi ni muhimu katika kuweka mazingira salama na kuwaepusha wananchi na mali zao dhidi ya madhara ya majanga hayo.

Jarida la Mtandaoni



SERIKALI YAZINDUA KITUO CHA OPERESHENI NA MAWASILIANO YA DHARURA MWANZA

Mwanza Serikali imezindua rasmi Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura cha Mkoa wa Mwanza, hatua kubwa inayolenga kuimarisha uratibu na ufanisi katika usimamizi wa maafa na majanga. Uzinduzi huo uliongozwa na aliyekua Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mheshimiwa Said Mtanda, aliye-bainisha kuwa kituo hicho kitakuwa nyenzo kuu ya kulinda maisha na mali za wananchi.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Mhe. Mtanda alieleza kuwa kituo hicho kitaleta mapinduzi kwa kuufanya mkoa uweze kufuatilia matukio ya dharura kwa karibu, kukusanya na kuchambua taarifa kwa wakati, pamoja na kuimarisha ush-irikiano kati ya wadau mbalimbali wa usimamizi wa maafa.

Alisisitiza kuwa kasi na usahihi wa mawasiliano ndio msingi wa kuokoa maisha wakati wa majanga. Kupitia kituo hicho, taarifa zote muhimu zitawafikia mamlaka husika kwa haraka ili kuwezesha maamuzi stahiki kuchukuliwa bila kuchelewa.

MWANZA YAONGEZA KASI KUZUIA VIFO VYA KUZAMA MAJI ZIWA VICTORIA



Serikali imeahidi kuendelea kuimarisha juhudi za kuzuia ajali na vifo vinavyotokana na kuzama maji katika Ziwa Victoria kupitia elimu, utafiti na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Taifa wa Kuzuia

Akizungumza kwenye Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kuzuia Kuzama Maji Duniani kwa niaba ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Bw. Henry Mwaijega alisisitiza kuwa usalama ziwani ni nguzo kuu ya kulinda uchumi unaotegemea uvuvi, usafiri na utalii.

Bw. Mwaijega alieleza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inaimarisha usimamizi wa maafa kwa kushirikiana na sekta binafsi, huku akisisitiza ukusanyaji wa takwimu, mafunzo ya uokoaji na matumizi ya makoti ya kuokoa maisha.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo ya Kiuchumi (EMEDO), Bi. Editrudith Lukanga, alisema wamefanikiwa kutoa mafunzo ya usalama kwa wavuvi na kusisitiza kuwa ushirikiano wa wadau wote ni muhimu katika kuzuia ajali ziwani.

Jarida la Mtandaoni

SIKUKUU YA WAKULIMA (NANENANE) MKOA WA MWANZA



Aliyekua Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mheshimiwa Said Mtanda, amewataka wakulima, wafugaji na wavuvi kutumia elimu na teknolojia walizojifunza kwenye Maonesho ya Nane Nane Kanda ya Ziwa Magharibi yaliyofanyika Nyamhongolo ili kuongeza tija. Alisisitiza kuwa uzalishaji lazima uzingatie mahitaji ya soko, matumizi ya mbegu bora, mbolea stahiki, na ushauri wa kitaalamu ili kujikwamua kiuchumi.

Ameziagiza kamati za maandalizi na viongozi wa Mwanza na Geita kuhakikisha elimu na bunifu hizo zinasambazwa hadi ngazi za vijitongoji, huku akitaka tathmini ifanyike ili kuboresha miundombinu ya viwanja hivyo kabla ya maonesho yajayo ya mwaka 2027.

Mhe. Mtanda alibainisha kuwa Serikali inaendelea kuwekeza kwa kutoa tani 12,420 za mbolea ya ruzuku na mikopo nafuu kwa vijana 56 wa mikoa hiyo katika sekta ya mifugo na uvuvi, ikizingatiwa kuwa sekta hizo zinaajiri asilimia 65 ya nguvu kazi ya Taifa.

MWENGE WA UHURU WAIFIKIA MIRADI 51 YA SHILINGI BILIONI 101.9 MWANZA

Aliyekua Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mheshimiwa Said Mtanda, ameupokea Mwenge wa Uhuru ukitokea mkoani Mara kupitia Wilaya ya Ukerewe, ambapo unatarajiwa kukimbizwa umbali wa kilometa 942.3 katika halmashauri zote nane za mkoa huo. Akizungumza kwenye hafla ya mapokezi iliyofanyika katika Viwanja vya Shule ya Msingi Muluseni, Mhe. Mtanda alibainisha kuwa mbio hizo za Mwenge zitaifikia na kuikagua miradi 51 ya maendeleo yenye thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni 101.9.

Miongoni mwa miradi hiyo, 11 itawekewa mawe ya msingi, 23 itazinduliwa rasmi, 8 itafunguliwa na mingine 9 itakaguliwa ili kujiridhisha na viwango vya ujenzi. Miradi hii inagusa sekta muhimu za afya, elimu, maji, barabara na madaraja, maendeleo ya jamii, uhifadhi wa mazingira pamoja na matumizi ya nishati safi, ikiwa ni sehemu ya mikakati ya Serikali ya kukuza uchumi na kuboresha huduma kwa wananchi.







CP HAMDUNI AKABIDHIWA RASMI OFISI

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mheshimiwa CP Salum Hamduni, amechukua rasmi mikoba ya uongozi wa mkoa huo na kuwataka watumishi na watendaji wa serikali kuongeza ufanisi, kuwajibika kwa nidhamu ya juu, na kusimamia kikamilifu ukusanyaji na matumizi ya mapato ya ndani kwa mujibu wa sheria na kanuni za fedha.

Akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano ya ofisi, Mhe. Hamduni alitumia fursa hiyo kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumwamini na kumteua kuongoza mkoa huo wa kimkakati. Aliahidi kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa na kushirikiana kwa karibu na viongozi pamoja na watendaji wote ili kuleta maendeleo kwa wananchi.





RC HAMDUNI ASHIRIKI USAFI SOKO KUU LA MWANZA, ATOA ONYO KWA WATENDAJI NA WAFANYABIASHARA





Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mheshimiwa CP Salum Hamduni, ameshiriki zoezi la usafi wa mazingira kwenye viunga vya Soko Kuu Mjini Kati Jijini Mwanza, ikiwemo kusafisha mitaro.

Akizungumza baada ya ukaguzi huo, alisema hali ya usafi jijini hapo si idhini na kuwataka wananchi wote kushiriki kikamilifu kufanya usafi kuanzia kwenye kaya zao ili kulinda afya na usalama wa mazingira.

Mhe. Hamduni pia alitoa maagizo makali kwa watendaji wa serikali kuacha utamaduni wa mazoea, urasimu, na vitendo vya kuomba rushwa wanapotoa huduma kwa wananchi. Aliwataka kufanya kazi kwa uwazi na kutoa huduma za haraka bila kuwazungusha wananchi.

Ameongezea, kwa kuagiza Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Halmashauri ya Jiji la Mwanza kuhakikisha hakuna mfanyabiashara anayerudi kufanyia biashara barabarani, akisisitiza maagizo hayo achukuliwe hatua za kisheria kupitia sheria ndogo za halmashauri.

KATIBU MKUU MAENDELEO YA JAMII ATEMBELEA OFISI YA MKUU WA MKOA



Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Bw. Eliakim Maswi, ametembelea Mwanza kujadili ujenzi wa Nyumba Salama (Safe Houses) za watoto wanaoishi mazingira magumu na Vituo vya Maendeleo ya Awali ya Mtoto (ECD) katika halmashauri 40 za Kanda ya Ziwa.

Bw. Maswi alieleza kuwa Wizara inashirikiana na Makatibu Tawala wa Mikoa ili kujenga umiliki wa pamoja na kuongeza usimamizi, huku wataalamu wakitumwa kutathmini miradi inayosuasua ili ijengwe kwa viwango na katika maeneo sahihi.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. CP Salum Hamduni, alisema wamekubaliana kutumia eneo la Bukumbi kwa miradi hiyo kwa kuwa ni kubwa, linamilikiwa na Serikali, na lipo nje ya jiji katika mazingira tulivu kwa ajili ya watoto.



KAMATI ZA MAAFA MWANZA ZATAKIWA KUIMARISHA MAANDALIZI YA KUKABILIANA NA MVUA ZA EL NINO

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mheshimiwa CP Salum Hamduni, amezitaka Kamati za Maafa za Mkoa na Wilaya kuimarisha ushirikiano katika kuweka mazingira salama na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu Salum Hamduni alisisitiza uwekaji wa mikakati madhubuti ya kuzuia na kupunguza madhara ya majanga hayo. Aliongeza kuwa mkoa umeanza kuchukua hatua za kimatendo ikiwa ni pamoja na kusafisha

Lengo ni kutathmini utayari wa Mkoa katika maandalizi ya kukabiliana na mvua za juu ya wastani (El-Nino), pia Mhe. CP bila vikwazo, huku elimu kwa umma kuhusu kuchukua tahadhari mapema ikiendelea kutolewa kote mkoani humo.



SAANANE NATIONAL PARK



Saanane National Park ni moja ya vivutio vya kipekee vya utalii nchini Tanzania, iliyopo katika Jiji la Mwanza, ndani ya Ziwa Victoria. Hifadhi hii inatoa fursa ya kipekee ya kufurahia mandhari ya kuvutia ya ziwa pamoja na uzuri wa mazingira ya asili.

Hifadhi hii inajulikana kwa kuwa na wanyamapori mbalimbali, wakiwemo swala, tumbili, nyani na wanyama wengine. Pia ni eneo linalofaa kwa shughuli za utalii kama kutazama wanyamapori, kupiga picha na kufurahia mandhari ya ziwa.







Kwa wakazi na wageni wanaotembelea Mwanza, Saanane National Park ni sehemu muhimu ya kutalii na kujifunza kuhusu uhifadhi wa mazingira na wanyamapori. Ni mahali panapounganisha asili, utalii na burudani katika mazingira ya kipekee ya Ziwa Victoria.



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza

Regional Drive, Mkabala na Ofisi za TRA

P.O. Box 119, Mwanza

mwanza.go.tz || rs_mwanza